KIJARIDA CHA KUELIMISHA JAMII JUU YA MASUALA MUHIMU YA

# USIMAMIZI WA ARDHI, UTAWALA, MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI NA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

HAKIARDHI Vol. 2. SEPTEMBA 2017 Land Rights Research & Resources Institute




## 1.0 MASUALA MUHIMU YA ARDHI

**1.1 Maana ya ardhi:** Kisheria ardhi inajumuisha vitu vyote vilivyo juu na chini ya uso wa nchi, vikiwemo majengo, uoto wa asili na maendelezo yote yaliyofanywa isipokuwa madini na bidhaa za mafuta na gesi. Mali hizo humilikiwa na serikali au watu binafsi na makampuni ambayo huingia mikataba ya kuzivuna kwa manufaa ya raia wote.

**1.2 Mgawanyo wa ardhi:** Ardhi ya Tanzania imegawanyika katika makundi matatu; ardhi ya kijiji, hifadhi na jumla. Ardhi ya kijiji ni ile iliyo ndani ya mipaka ya kijiji kwa mujibu wa sheria mbalimbali. Ya hifadhi ni ile iliyotengwa kwa matumizi maalum kama vile wanyama pori, milima, misitu, ardhi oevu, na hifadhi za barabara. Ardhi ya jumla ni ile inayobaki baada ya kuondoa ya kijiji na ya hifadhi.

**1.3 Upatikanaji wa ardhi:** Unaweza kupata ardhi kwa kumilikishwa na serikali, kurithi kwa ndugu, kununua au kupewa zawadi.

**1.4 Kumiliki ardhi kisheria:** Umiliki wa ardhi uko wa aina mbili. Kwanza ni umiliki wa kimila na pili, umiliki kwa njia ya hatimiliki. Hata hivyo, wanaomiliki kimila nao hupewa cheti cha hakimiliki ya kimila (CCRO) chenye hadhi sawa kabisa na hatimiliki.

**1.5 Ugawaji na umilikishaji wa ardhi:** Ardhi ya kijiji husimamiwa na hugawiwa na Halmashauri ya kijiji kwa idhini ya Mkutano Mkuu wa kijiji.Ardhi ya hifadhi hutengwa na Wizara ya ardhi kwa kushirikiana na mamlaka za hifadhi husika na husimamiwa na mamlaka hizo.

Ugawaji wa ardhi ya jumla hufanywa na Halmashauri ya Wilaya na Manispaa kwa waombaji wa maeneo ambao hupewa hatimiliki. Kamishina wa ardhi ndiye msimamizi na mwangalizi mkuu wa makundi yote na ndiye hutunza taarifa na nakala za hati zote.

Land Rights Research & Resources Institute HAKIARDHI

***1.6 Haki za mmiliki wa ardhi:*** Kwanza ana wajibu wa kuitunza na kuiendeleza. Pili ana haki ya kutumia moja kwa moja kwa kilimo, ufugaji, uchimbaji madini au kwa kutumia hatimiliki kupata manufaa mengine yatokanayo na umiliki wake. Kwa mfano, mtu anaweza kuweka rehani hatimiliki yake akapata mkopo benki na kuitumia kwa shughuli nyingine.

***1.7 Haki za mmiliki wa ardhi inapotwaliwa:*** Ardhi yoyote ikihitajika kwa shughuli za kimaendeleo, kamili, ya haki na kwa wakati kwa mujibu wa sheria. Fidia inajumuisha ardhi tupu, maendelezo, posho za iliyotwaliwa ilikuwa inatumika kwa shughuli hizo.


## 2.0 USIMAMIZI WA ARDHI YA KIJIJI

***2.1 Halmashauri ya Kijiji:*** Halmashauri ya Kijiji ndiyo yenye dhamana ya usimamizi wa ardhi ya kijiji kwa niaba ya wanakijiji na wakazi wengine wanaoishi katika kijiji na kunufaika na ardhi ya kijiji. Itawajibika kutoa taarifa kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji na kupokea mawazo yao kuhusiana na utawala na uendeshaji wa ardhi ya kijiji katika vikao vya kawaida vya Mkutano Mkuu wa Kijiji.

***2.2 Kamati ya Maamuzi ya Kijiji:*** Kamati inaundwa na wajumbe wasiopungua 6 na wasiozidi 9 kati yao wanawake wasipungue 3. Majukumu ya Kamati ni pamoja na kuweka mipaka ya ardhi na kushughulikia maslahi yaliyo katika ardhi inayohusika katika kutolewa maamuzi. Kutenga, au kuweka akiba ya ardhi au kutoa mipaka ya haki ya njia na haki zingine za kutumia njia ambazo itaziona ni muhimu kwa umiliki bora wa ardhi. Kulinda maslahi ya wanawake, watu wasiokuwepo, watoto wadogo na walemavu.

***2.3 Mkutano Mkuu wa Kijiji:*** Ni chombo chenye madaraka na mamlaka ya juu kuhusu masuala yote ya kijiji yakiwemo masuala ya ardhi. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kijiji ni wanakijiji wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea na wakazi wa kijiji husika. Majukumu yake ni pamoja na; Kuthibitisha, kukubali au kukataa maombi ya ardhi yaliyowasilishwa na Halmashauri ya Kijiji. Kuthibitisha au kukataa wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji na wajumbe wa Kamati ya Maamuzi ya Kijiji, waliopendekezwa na Halmashauri ya Kijiji. Kupitisha mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji kama ulivyopendekezwa na Kamati Shirikishi ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji (VLUM) na Kamati Shirikishi ya Mpango wa Matumizi ya ardhi ya Wilaya (PLUM).

***2.4 Halmashauri ya Wilaya:*** Halmashauri ya Wilaya ina jukumu la kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Halmashauri ya Kijiji kuhusiana na usimamizi na matumizi ya ardhi ya kijiji.




***2.5 Kamishna wa Ardhi:*** Kamishna wa ardhi ana majukumu ya kutoa maelekezo kwa Halmashauri ya Kijiji kuhusu usimamizi wa ardhi ya kijiji kwa mujibu wa fungu la 8(7) la Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999. Kuweka saini na lakiri cheti cha ardhi ya kijiji. Kutunza daftari la vyeti vya ardhi za kijiji. Kutoa ushauri kwa Halmashauri ya Kijiji na kwa Rais juu ya uhawilishaji wa ardhi ya kijiji baada ya kupokea muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kijiji na ushauri wa Halmashauri ya Wilaya.

## 3.0 UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

***3.1 Maana ya migogoro ya ardhi:*** Migogoro ya ardhi ni ugomvi baina ya watu au makundi ya watu wanaogombania rasilimali kama vile ardhi, malisho au maji na kusababisha athari kubwa zikiwemo vifo vya watu na mifugo, uharibifu wa mali na miundombinu na kukosekana kwa usalama katika jamii.

***3.2 Vyanzo vya migogoro ya ardhi:*** Migogoro ya ardhi inasababishwa na kutofahamika kwa sheria kwa katika maamuzi, mapungufu ya sera na sheria, kupanuka kwa miji, ongezeko la watu na mifugo na kugunduliwa kwa maliasili, kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi.


***3.3 Utatuzi wa migogoro ya ardhi:*** Kwa njia za kawaida ambazo huhusisha mila za wenyeji husika au kiutawala kufuata ngazi za kiserikali. Hata hivyo, Sheria ya Mabaraza na Mahakama za Ardhi namba 2 ya 2002 imeunda vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa. Vyombo hivyo ni;

***(i) Baraza la Ardhi la Kijiji:*** Linaundwa na wajumbe 7 kati yao wanawake ni 3. Wajumbe huteuliwa na halmashauri ya Kijiji, kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji, hudumu kwa miaka 3 na huweza kurudia tena kwa miaka 3 tu. Sifa za wajumbe; awe mwanakijiji, kuanzia miaka 18, asiye na wadhifa mwingine katika serikali na asiyewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai. Baraza hutumia njia za kimila kusuluhisha tu ili kuleta mapatano na wala siyo kutoa hukumu wala kulipiza faini au fidia.

***(ii) Baraza la Kata:*** linaundwa na wajumbe kati ya 4 hadi 8 kati yao 3 wanawake. Wajumbe huteuliwa na Kamati ya Mandeleo ya Kata miongoni mwa vijiji vinavyounda kata husika. Wajumbe hudumu kwa miaka 3 na huweza kurudia tena kwa miaka 3 tu. Mjumbe sharti awe na umri kuanzia miaka 18, mkazi mwenyeji wa kata husika, asiye kiongozi wa serikali na asiyewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai. Baraza lina uwezo kifedha wa mashauri ni hadi milioni 3. Mtu anaweza kukata rufaa kwenda Baraza la Ardhi na nyumba la Wilaya ndani ya siku 45 tangu hukumu.

***(iii) Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya:*** huundwa na Wizara wa Ardhi kwa kumteua Mwenyekiti ambaye ana sifa ya digrii ya sheria na ambaye huapishwa na Mkuu wa Mkoa husika. Mkuu wa mkoa huteua wazee 7 na wanawake wasipungue 3 wa baraza kumsaidia mwenyekiti japo halazimiki kufuata ushauri wao. Baraza hutoa hukumu na kulipiza faini na ya shilingi milioni 40 kwa mali inayohamishika au 50 kwa mali isiyohamishika. Rufaa kutoka baraza hili kwenda mahakama kuu ni ndani ya siku 60 tangu hukumu kutolewa.

***(iv) Mahakama kuu*** husikiliza kesi zote zinazotokanana na rufaa ya ngazi za chini na zinazoanzia pale pale. **Mahakama ya Rufaa** ndiyo ngazi ya mwisho ya vyombo hivi ambayo hupokea kesi za warufani ambao hawakuridhika na maamuzi ya ngazi za nchini





## 4.0 MFUMO WA UTAWALA NA USIMAMIZI RASILIMALI VIJIJINI

***4.1 Muundo wa serikali:*** Mfumo wa Serikali ya Tanzania una muundo wa utawala uliogawanyika katika serikali kuu na serikali za mitaa. Serikali kuu huanzia kwa Rais, Baraza la Mawaziri, ngazi ya Mkoa, Wilaya na Tarafa. Serikali za mitaa huongozwa na mamlaka za halmashauri za miji na wilaya, mwisho wa serikali za mitaa ni ngazi ya kijiji.

***4.2 Vyombo vya Utawala Kijijini:*** Kijiji kina vyombo vikuu viwili ambavyo ni Mkutano Mkuu wa kijiji na Halmashauri ya Kijiji. Halmashauri ya kijiji ni chombo cha utendaji kupitia kamati 3 za kudumu za ulinzi na usalama, huduma za jamii, uchumi, mipango na fedha. Kuna aina 3 za vikao vya mikutano Mikuu ya Vjiji ambavyo ni kikao cha kawaida kila baada ya miezi 3, kikao cha uchaguzi kila baada ya miaka 5 na kikao cha dharura.

***4.3 Majukumu ya mkutano mkuu wa Kijiji:*** Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za utekelezaji za kijiji, mapato na matumizi, mapendekezo ya kodi, sheria ndogo ndogo na ugawaji wa ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kijijini.

***4.4 Majukumu ya Halmashauri ya kijiji:*** Ni chombo kinachoundwa na wajumbe 15 hadi 25 waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Halmashauri ya kijiji ndiyo serikali ya Mtendaji wa kijiji. Kazi zake ni kupanga mipango ya maendeleo na kutoa mapendekezo kwenye mkutano mkuu, kutekeleza maamuzi ya mkutano mkuu na vyombo vya juu. Vikao vya halmashauri ya kijiji hufanyika kila mwezi kikao kimoja.




## 5.0 UANDAAJI NA USIMAMIZI WA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

**5.1 Maana ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Kijijini:** Ni utaratibu wa kutathmini na kupendekeza namna mbalimbali za matumizi ya ardhi na maliasili ili kuinua hali ya maisha ya wanakijiji na kuondoa umaskini. Ili mpango uwe na tija ni sharti uandaliwe kwa kushirikisha makundi mbalimbali yaliyopo katika kijiji.

**5.2 Faida za Mpango wa Matumizi ya Ardhi:** Kupunguza migogoro ya ardhi baina ya makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi na maliasili. Kutoa uhakika wa milki za ardhi kwa wananchi kupitia hakimiliki za kimila. Kuboresha matumizi ya ardhi kwa kugawa ardhi katika makundi mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi pamoja na kusaidia utunzaji wa mazingira na hasa vyanzo vya maji, misitu na wanyamapori kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### 5.3 Mamlaka za Upangaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Ngazi ya Taifa

**(i) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi :**

Inaundwa na wajumbe wasiopungua 5 na wasiozidi 10 kati yao wanawake wasipungue 3 kutoka sekta mbalimbali kama vile ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi; kilimo na mifugo, nishati au madini; serikali za mitaa; maji; afya; maliasili; utalii; uvuvi; sheria; fedha; mazingira; uchumi na mipango. Wajumbe hao wanateuliwa na Waziri mwenye dhamana ya ardhi na kuongozwa na Mwenyekiti wa Tume ambaye huteuliwa na Rais. Majukumu ya Tume ni kuandaa mpango wa kitaifa wa matumizi ya ardhi, kuandaa mipango kabambe ya kikanda ya matumizi ya ardhi pamoja na kuratibu, kusimamia na kutoa mwongozo wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya na vijiji.

**(ii) Ngazi ya Wilaya:** Halmashauri ya Wilaya itaunda Kamati Shirikishi ya Mpango waMatumizi ya Ardhi (PLUM) yenye wajumbe 6 hadi 8 kutoka idara zinazohusiana na ardhi kama vile kilimo, mifugo, maliasili, ardhi na maendeleo ya jamii. Timu ya PLUM ina wajibu wa kuratibu na kuwezesha uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi Wilayani na kuziwezesha Halmashauri za Vijiji na kuunda Kamati za Matumizi ya Ardhi za Kijiji (VLUM) yenye wajumbe kati ya 5 mpaka 10 kutoka miongoni mwa wanakijiji.

**(iii) Ngazi ya Kijiji:** Halmashauri ya Kijiji huandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya kijiji kupitia Kamati ya Usimamizi na Matumizi ya Ardhi. Katika ngazi hii ni lazima mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji uwe ni mchakato shirikishi unaozingatia ushirikishwaji wa wananchi kikamilifu kupitia Mikutano Mikuu ya Vijiji au mwananchi mmoja mmoja.

**Upangaji wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji:** Uandaaji wa mpango wa matumizi ya kijiji sharti uzingatie ugawaji wa ardhi kwa matumizi mengine yoyote kuendana na mahitaji ya watumiaji kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa na Wizara ya Ardhi kama ifuatavyo;

- Maeneo ya makazi na huduma za jamii; Mfano shule, zahanati,ofisi masoko, maduka nyumba za ibada barabara na makaburi.
- Maeneo ya kilimo; Maeneo ya kilimo cha mazao ya kudumu, mazao ya msimu, mazao ya umwagiliaji, kilimo cha misitu.
- Maeneo ya kuchungia; Maeneo kwajili ya malisho, nyika, njia za mifugo huduma za mifugo kama vile majosho na maji.
- Maeneo ya misitu; Huusisha mimea asilia yenye miti mingi, matumizi ya mbao, majengo, kuni, mkaa, asali, mitishamba, na uhifadhi wa mimea asilia.

Dreikönigsaktion Hilfswerk der Katholischen Jungschar
Welthaus DIÖZESE GRAZ-SECKAU
HORIZONT3000
WITH FUNDING FROM AUSTRIAN DEVELOPMENT COOPERATION

HAKIARDHI
KWA MAWASILIANO ZAIDI TUMIA ANUANI ZIFUATAZO
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi –HAKIARDHI
Kitalu Na.236 Block 47 Sinza Mori, S.L.P 75885, Dar es Salaam,
Simu +255 22 2771360/ 0784 646752, Nukushi: +255 22 2771362,
Baruapepe: info@hakiardhi.org, Tovuti: www.hakiardhi.org